Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji

ISO 9001 : 2015 Certified

HALIUZWI

# Newsletter

Februari 2024

ISSN 1821 - 7273 TOLEO NA. 37

# EWURA yahamasisha uwekezaji kwenye vituo vya Gesi Asilia iliyokandamizwa



PERUZI HAPA

*Kauli Mbiu: "Udhibiti wa Haki kwa Matokeo CHANYA - IMPACT"*

**Toleo Lililopita**





## BODI YA WAHARIRI

**MWENYEKITI**
Dkt. James Andilile

**MHARIRI**
Bw. Titus M. Kaguo

**MHARIRI MSAIDIZI**
Bw. Wilfred Mwakalosi

**WAANDISHI**
Bi. Asiatu Msuya
Bi. Tobietha Makafu



**MAKAO MAKUU YA EWURA**
Jengo la EWURA,
3 Mtaa wa EWURA,
41104 Tambukareli,
S..L.P. 2857, Dodoma, Tanzania.
Simu: +255 26 2 329 002-4
Nukushi: +255 26 2329005,
Barua Pepe: info@ewura.go.tz
Simu ya BURE: 0800110030
***www.ewura.go.tz***

ewuratanzania

ewuratv


# YALIYOMO


Kutoka Dawati la Mkurugenzi Mkuu ........ 3

Kutoka Dawati la Mhariri ........ 4

EWURA: Wekezeni kwenye Gesi Asilia ........ 5

Zingatia yafuatayo kupunguza gharama za maji, umeme ........ 6

Bodi ya EWURA yatembelea miundombinu ya Gesi Asilia ........ 7

Mikataba ya kuuziana Mafuta huimarisha Huduma- EWURA ........ 8

Ujenzi wa Bomba jipya la Tazama upo mbioni ........ 9

RC SHINYANGA: Itumieni EWURA, sasa imesogea Kanda ya Magharibi ........ 10

Ushirikishwaji wa EWURA kwa wadau wa habari waleta mafanikio ........ 11

Mamlaka za Maji zatakiwa kuelimisha wateja kuhusu huduma ........ 12




**PICHA YA MBELE:**
*Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Doto Biteko, akikaribishwa na Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Dkt. James Andilile alipowasili katika ofisi za EWURA, Dar es Salaam kwa mara ya kwanza baada ya uteuzi wake Septemba 2023..*

# Kutoka Dawati la **Mkurugenzi Mkuu**



**Dkt. James Andilile**

***Mpenzi Msomaji Heri ya mwaka Mpya 2024!***

*Nina furaha kwangu kupata nafasi hii ya kukukaribisha tena kulisoma jarida letu kwa kipindi kinachoishia Desemba 2023.*

*Kwa mtazamo wa Kiudhibiti, kipindi cha mwisho wa mwaka 2023 kilikuwa kipindi kizuri, huku watu wakisafiri kwenye mapumziko ya mwisho wa mwaka bila kukabiliwa na ukosefu wa huduma tunazozidhibiti.*

*EWURA itaendelea kutekeleza majukumu yake ili kuyafanya mazingira ya uwekezaji yawe bora zaidi, huku ikiendeleza falsafa yake ya maamuzi shirikishi na kuhakikisha kwamba maamuzi yoyote ya kiudhibiti yanakuwa ya haki, yanayotabirika na yenye mtazamo wa kibiashara.*

*Wakati tunalenga kufanya kazi na jamii inayoheshimu utawala bora, ni matamanio yetu kuwa kila mtu awe na ufahamu wa kile tunachofanya na mipango yetu ya baadaye. Na hili, kwa hakika, ndiyo lengo letu kuu hasa kwa kuwa na Jarida hili—kuhabarisha na kuongeza uelewa wa shughuli za kiudhibiti, kwa watoa huduma na watumia huduma pia.*

*Mwisho japo si kwa umuhimu, nachukua fursa hii tena kuwatakia Heri ya Mwaka Mpya 2024 na mafanikio tele!*

# Kutoka Dawati la **Mhariri**



**Titus M. Kaguo**

***Mpenzi Msomaji wetu!***

***Heri ya Mwaka Mpya 2024!***

*Kwa unyenyekevu na heshima kubwa mimi na wenzangu tunakuletea tena nakala ya jarida letu, ikiwa ni ishara ya kuendelea kukutumikia tena mwaka huu wa 2024! Tunakukaribisha tena kusoma na kutoa maoni yako kwenye jarida letu, ambalo kimsingi ni sehemu ya utekelezaji wa jukumu la EWURA la kuongeza uelewa na ufahamu wa umma kuhusu sekta zinazodhibitiwa.*

*Kwa kawaida, Jarida hili hutolewa kila baada ya miezi mitatu, ambapo toleo hili lina masuala kadha wa kadhaa ya kisekta kuanzia mwezi Oktoba hadi Disemba 2024. Kuna Makala mbalimbali zitakazokuvutia kusoma kama vile namna ambavyo unaweza kupunguza gharama za kila mwezi za maji na umeme, umuhimu wa mikataba ya kuuziana mafuta, ziara ya hivi karibuni ya Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA kwenye mikoa ya Lindi na Mtwara, ujenzi wa bomba jipya la mafuta kwenda Zambia, na nyingine kem kem!*

*Vile vile, napenda kutumia fursa hii kuitambulisha mitandao yetu ya kijamii ya ewuratanzania (Facebook), ewuratanzania (X), ewuratanzania (Instagram) na EWURATV (online TV). Kupitia mitandao hii, tunakutana na jamii zetu na wadau kwa ujumla ambapo tunakuwa na majadiliano yenye tija na kupata mrejesho kuhusu mambo mbalimbali.*

*Karibu Sana!*

# EWURA: Wekezeni kwenye Gesi Asilia

***Na Asiatu Msuya***

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imewashauri wawekezaji kuwekeza kwenye vituo vya gesi asilia iyogandamizwa (CNG) kwani soko bado ni kubwa ikilinganishwa na vituo vya mafuta.

EWURA imesema changamoto zinazoikabili sekta hiyo ikiwamo uwekezaji mdogo katika usambazaji wa nishati hiyo ya kuendesha magari, viwanda na matumizi ya nyumbani na shughuli nyingine za uzalishaji zitakwisha iwapo wananchi wenye uwezo watatumia fursa zilizopo kwenye sekta kuwekeza.

Mkurugenzi wa Gesi Asilia EWURA, Mha. Poline Msuya alisema hivi karibuni kuwa tayari serikali imeandaa kanuni za uendeshaji wa CNG zinazosimamiwa na EWURA, lakini tatizo bado ni mwamko mdogo wa uwekezaji, hivyo EWURA kwa kushirikina na wadau wengine inaimarisha kampeni za uhamasishaji, ili kuvutia wawekezaji.

"Serikali imeweka mazingira wezeshi, na tunachukua hatua madhubuti kuhakikisha uwekezaji kwenye CNG unashamiri ili tuimarishe upatikanaji wa huduma na kurahisisha maisha ya Watanzania," alisema Dkt. Andilile. Baadhi ya wadau wa ngazi ya serikali wanaohusika kutoa suluhu ya changamoto zinazokabili mnyororo wa uwekezaji kwenye CNG ikiwa ni pamoja na Wizara za Fedha, Nishati na Ardhi, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Baraza la Usimamizi wa Mazingira, Shirika la Utafiti wa Petroli,

Shirika la Viwango na Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam, watakutana hivi karibuni katika kongamano la kujadili changamoto, na namna ya kuipeleka mbele sekta ya Gesi Asilia.

Fursa za uwekezaji katika CNG ni pamoja na kituo mtandao (matumizi ya umma/au ya kibinafsi); kituo cha kujaza CNG nje ya mtandao (matumizi ya umma/ binafsi); kituo dada cha CNG (kwa matumizi ya viwanda, biashara, uzalishaji wa umeme au katika kaya); usafirishaji wa CNG; karakana za kubadili mifumo ya magari kuweza kutumia CNG; wahakiki/wakaguzi wa mifumo ya CNG na magari yaliyobadilishwa mfumo (teksi, mabasi na malori). Kwa sasa, vipo vituo vitano (5) vinavyotoa huduma ya gesi asilia iliyokandamizwa kwenye magari, taasisi saba (7) zinazotumia CNG, viwanda zaidi ya 30, nyumba 1,552, vituo 10 vya kubadilisha mifumo ya magari na magari 3,758 yaliyobadili mfumo ili kutumia CNG katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Lindi na Mtwara.

EWURA hutoa vibali vya ujenzi wa miundombinu ya CNG ndani ya siku 30 na leseni za uendeshaji ndani ya siku 60 baada ya kupokea maombi kamili. Gharama za kibali cha ujenzi ni shilingi milioni tano na leseni shilingi 1,500,000/ ambayo hudumu kwa miaka isiyopungua 25. Maombi yote ni kupitia mfumo wa leseni ujulikanao kama LOIS unaopatikana kwenye tovuti ya Mamlaka www.ewura.go.tz.

# Zingatia yafuatayo kupunguza gharama za maji, umeme

*Na Mwandishi Wetu*

Baadhi ya watumiaji wa maji na umeme wamekuwa wakilalamika gharama kubwa wanazotozwa kwa kutumia huduma hizo. Hata hivyo, utafiti usio rasmi unaonesha kaya nyingi hazina utaratibu mzuri wenye kujali matumizi sahihi ya huduma hizo. Makala hii fupi inakusudia kuelimisha watumia huduma namna bora ya kutumia maji na umeme.

## 1. Matumizi salama na sahihi ya Maji

Kwa matumizi ya maji, hakikisha yafuatayo:

- Wakati wote, hakikisha mfumo mzima wa mabomba ya maji hauna eneo linalovuja, hii ni pamoja na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye viungo, mabafu na vyoo vya kuvuta
- Namna bora ya kuosha vyombo ni kutumia maji yaliyo kwenye chombo, na si yanayotiririka moja kwa moja kutoka bombani, kwani mtindo huu hutumia maji mengi
- Zingatia matumizi bora ya vitufe vya kubonyeza kwenye choo cha kuvuta; kitufe kidogo ni kwa ajili ya haja ndogo
- Tanki la choo (flush tank) lirekebishwe ili kitumie maji ya kadiri
- Unaposafisha kinywa, kinga maji kwenye chombo badala ya kuacha maji yatiririke kutoka bombani
- Unapotaka kuoga maji moto kwenye bomba la mvua, usiache maji baridi yakamwagika tu, eti kwa sababu unasubiri maji ya moto yaanze kutoka
- Fuatilia hesabu inayooneshwa kwenye dira au mita yako ya maji, na uwianishe na hesabu inayoletwa na Mamlaka ya Maji. Ukiwa na mashaka na usahihi wake, toa taarifa kwa mtoa huduma wako mara moja.
- Jitahidi kuhifadhi maji ya mvua ili yakusaidie kwenye matumizi kama chooni, kusafisha vyombo, nyumba nk na hatimaye kukupunguzia gharama za maji
- Ifundishe kaya yako mambo ya msingi kama ilivyoainishwa hapa.

## 2. Matumizi salama na sahihi ya Umeme

Mtumiaji umeme anapaswa kuzingatia utumiaji salama na sahihi wa nishati hiyo ili iwe huduma salama kwa maisha ya watu na mali zao. Mtumiaji umeme anapaswa kuzingatia haya wakati wote:

- Tumia fundi mwenye leseni iliyotolewa na EWURA kwa na ubora uhakika wa kazi za kufunga mifumo ya umeme majumbani
- Fahamu viwango vya matumizi ya umeme kwa kila kifaa cha umeme unachonunua au kutumia
- Fuata maelekezo ya mtoa huduma hasa kwa orodha ya vifaa vyako vya umeme
- Tumia taa zenye kiwango cha mwanga unaohitajika eneo husika.
- Eneo lisilohitaji taa kuwaka, mfano chumba ambacho hakina mtu, basi taa husika zizimwe.
- Taa za nje zizimwe kila kunapokucha. Ikiwezakana, tumia kifaa cha kusaidia taa kujizima na kujiwasha zenyewe (photocell).
- Piga pasi nguo nyingi kwa mara moja, badala ya nguo moja moja kila siku, kwani hii itasaidia kupunguza matumizi ya umeme
- Ukubwa wa kitako cha sufuria uwiane na ukubwa wa jiko la umeme, ili kuzuia joto lisipotee nje ya kitako cha sufuria. Funika sufuria.

- Fanya ukaguzi wa mfumo wa umeme darini na kwingineko angalau mara moja kwa miaka mitano; kwani kufanya hivyo kunasaidia kubaini mapema matatizo yanayoweza kusababisha ajali za moto
- Vilinde vifaa vinavyotumia umeme kwa kutumia vidhibiti umeme (stabilizer, voltage regulator)
- Unapomaliza matumizi ya kifaa cha umeme, zima swichi na kuchomoa waya husika kutoka kwenye soketi, kwani kifaa huendelea kutumia kiasi fulani cha umeme hata pale ambapo kinakuwa kimezimwa
- Friji tupu izimwe, kwani inapofanya kazi kama ina vitu vichache sana, ndiyo inavyotumia umeme mwingi. Friji tupu, inapufunguliwa na kufungwa, hujitahidi kupooza hewa nyingi ya joto iliyoingia mlango wa friji ulipokuwa wazi.

# Bodi ya EWURA yatembelea miundombinu ya Gesi Asilia

***Na Mwandishi Wetu***

BODI ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imesema imeridhishwa na jitihada za serikali kuhakikisha miundombinu ya gesi asilia inapewa kipaumbele katika suala la ulinzi dhidi ya hujuma zozote zinazoweza kufanywa na adui.

Mwenyekiti wa Bodi hiyo Prof. Mark Mwandosya, alimweleza Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Mh. Kanali Ahmed Abbas Ahmed wakati Bodi hiyo ilipomtembelea ofisini kwake hivi karibuni kuwa usalama wa miundombinu ya gesi asilia, au yoyote ile, ni jambo la msingi sana katika kuhakikisha maendeleo endelevu.

“Eneo hili la kusini mwa nchi yetu ni la kimkakati...ni jambo la kupongezwa, kuona namna ambavyo serikali imeimarisha ulinzi kwa miundombinu ya gesi asili kwa manufaa ya watu wake,” alisema Prof. Mwandosya.

Kanali Abbas alisema licha ya hali kuonekana hivyo, mkoa wa Mtwara bado unakabiliwa na changamoto za barabara, umeme na maji kwenye maeneo mengine ya kimkakati. “Serikali imeweka mipango thabiti kuhakikisha kuwa hivi karibuni itaitekeleza mipango hiyo ili kuhakikisha kuwa upatikanaji wa umeme unakuwa wa uhakika, ikiwa ni pamoja na usimamizi wa karibu wa mradi wa maji wa Makonde ambako kasi ya utekelezaji wa mradi huo hairidhishi,” alisema. Katika majadiliano na Bodi, viongozi hao walikubaliana kwa serikali kutoa msukumo kwa utekelezaji wa mpango wa uvunaji wa maji ya mvua, utaratibu ambao utasaidia kupunguza tatizo la upatikanaji maji na kupunguza uharibifu wa barabara na miundombinu mingine.

Katika ziara hiyo, Bodi ya EWURA ilitembelea Kisiwa cha Songo Songo, mkoani Lindi, ambako ilikagua miundombinu ya Kampuni ya Taifa ya GASCO, na ile ya PanAfricanEnergy na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mkuu wake Bw. Andy Hanna. Mkoani Mtwara, Bodi hiyo ilitembelea Kampuni ya Maurel & Prom katika eneo la visima vya gesi la Mnazi Bay, na Kampuni ya Tanzania Petroleum Development Corporation (TPDC) katika eneo la Madimba. Katika maeneo yote hayo, licha ya kujionea hali ya miundombinu, Bodi ilikutana na kufanya mazungumzo na wataalam ili kufahamu changamoto za kiutendaji na namna ambavyo Bodi inaweza kusaidia utatuzi wake.

# Mikataba ya kuuziana Mafuta huimarisha Huduma-EWURA

***Na Asiatu Msuya***

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imesema wafanyabiashara ya mafuta nchini wanatakiwa kutekeleza wajibu wao kisheria wa kuingia mikataba ya kibishara na wauzaji wa jumla wa bidhaa hiyo ili kuimarisha na kurahisisha upatikanaji wa uhakika wa huduma kwa wananchi.

EWURA imesema kwa mujibu wa kifungu cha 143 cha Sheria ya Petroli, Sura Na. 392, wafanyabiashara wanapaswa kuhakikisha wanatekeleza masharti ya leseni zao yanayowataka kutoharibu mnyororo wa upatikanaji wa huduma kwa kununua kiwango cha mafuta kinachokidhi mahitaji ya eneo husika na kuuza mafuta hayo kila siku kwa wateja.

Mkurugenzi wa Petroli EWURA, Bwa. Gerald Maganga alisema hivi karibuni kuwa kila kituo cha mafuta kinatakiwa kuwa na mkataba au mikataba na wafanyabiashara wa jumla na kuhifadhi nyaraka zote kwa ajili ya rejea na ukaguzi wa EWURA ambao hufanyika mara kwa mara kufuatilia utendaji na utii wa sheria na miongozo. "Nitumie fursa hii kuwaagiza wafanyabiashara ya mafuta kuhakikisha wanaingia mikataba husika ili kuwa na uhakika wa kupata bidhaa hiyo wakati wote," alisema Bw. Maganga.

Hivi karibuni, EWURA iliviadhibu baadhi ya vituo vya mafuta baada ya kubainika pamoja na mambo mengine, kutofanya biashara kwa maelezo ya kukosa mafuta kutoka kwa wauzaji wa jumla huku EWURA ikiwa imejiridhisha kuwepo mafuta kwenye maghala ya kuhifadhi mafuta.

Kwa wafanyabiashara kutokuwa na mikataba na wauzaji wa jumla, hali hii husababisha kukosekana huduma kwa baadhi ya maeneo.

Mpaka sasa EWURA imetoa jumla ya leseni 2506 za vituo vya rejereja vya mafuta ikiwamo vituo 284 vya maeneo ya vijijini. Maombi ya leseni hufanyika kwa mfumo wa LOIS unaopatika katika tovuti ya Mamlaka www.ewura.go.tz.

EWURA inatoa rai kwa wamiliki wa vituo vya mafuta vya rejareja kuwa na mikataba ya kibiashara na yeyote atakayeayekiuka atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria ikiwamo kufuta leseni ya biashara.

# Ujenzi wa Bomba jipya la Tazama upo mbioni

***Na Tobietha Makafu***

Ujenzi wa Bomba jipya la kusafirisha mafuta kutoka Dar es Salaam, Tanzania hadi Ndola Zambia, likitumia mkuza wa bomba la TAZAMA litakalokuwa na urefu wa kilomita 1,710 na uwezo wa kusafirisha mita za ujazo tani milioni 4, upo mbioni kuanza.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko, amesema hayo tarehe 29.01. 2024 alipokutana na Waziri wa Nishati wa Zambia Mhe. Peter Kapala, jijini Dodoma kujadili utekelezaji wa mapendekezo ya ujenzi wa bomba hilo.

Makubaliano ya ujenzi wa bomba hilo yalifikiwa kwa mara ya kwanza baina ya Rais mstaafu wa Zambia, Mhe. Edgar Changwa Lungu na aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dr. John Pombe Magufuli, mwaka 2016.

"Kikao cha leo ni matokeo ya ziara ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, nchini Zambia, mwezi Oktoba 2023, ambapo walijadili na Rais wa Zambia, Mhe. Hakainde Hichilema, kuhusu utekelezaji wa ujenzi wa bomba jipya la TAZAMA," alisema Dkt. Biteko.Kikao kilijumuisha wataalam wa EWURA, PURA na TPDC, taasisi ambazo hutekeleza majukumu mbalimbali kwenye sekta ya petroli nchini. Tayari Kamati ya ufundi inayojumuisha wataalamu wa mafuta, sheria na udhibiti uchumi kutoka Tanzania na Zambia imeundwa ili kufanikisha shughuli za awali za ujenzi wa bomba hilo ikiwamo kutengeneza hadidu za rejea, kufanya upembuzi yakinifu pamoja na uchambuzi wa athari za mazingira na kijamii katika mradi huo. Kamati hiyo itaongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mha. Felchesmi Mramba.





*Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko (watano kulia) katika picha ya pamoja na ujumbe kutoka Wizara ya Nishati Zambia, ukiongozwa na Waziri wa Nishati Zambia Mhe. Peter Kapala (watano Kushoto) na ujumbe kutoka Wizara ya Nishati Tanzania, kutoka kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa TPDC, Bw. Mussa Makame, Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Dkt. James Andilile, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mha. Felchesmi Mramba na Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Judith Kapinga, mara baada ya mawaziri hao kufanya mazungumzo kuhusu mapendekezo ya ujenzi wa bomba jipya la mafuta linalotarajiwa kujengwa, kuanzia Dar es Salaam hadi Zambia..*

# RC SHINYANGA: Itumieni EWURA, sasa imesogea Kanda ya Magharibi

***Na Tobietha Makafu***

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Mhe. Christina Mndeme, amekaribisha uanzishwaji wa ofisi ya EWURA Kanda ya Magharibi itakayohudumia mikoa ya Shinyanga, Katavi, Tabora na Kigoma, yenye ofisi zake mkoa wa Tabora.

Mhe. Mndeme ameyasema hayo wakati Kaimu Meneja wa EWURA Kanda ya Magharibi, Mha. Walter Christopher, alipofanya ziara ya kikazi, ofisini kwake kuitambulisha ofisi ya EWURA Kanda ya Magharibi na kujadili utekelezaji wa shughuli za udhibiti wa huduma za nishati na maji katika kanda hiyo.

"Ninaipongeza EWURA kwa kusogeza ofisi karibu na wananchi, kwani itarahisisha utatuzi wa changamoto mbalimbali katika huduma za nishati na maji na kuhakikisha huduma zinapatikana kwa wakati na gharama sahihi," alisema Mhe. Mndeme.

Mhe. Mndeme aliwataka Wananchi na hasa wana Shinyanga kutumia fursa hiyo kwa kuitumia EWURA kutatua changamoto wanazokumbana nazo katika sekta za nishati na maji, na ambazo watoa huduma wameshindwa kuzitatua.

Hivi Karibuni ofisi ya EWURA Kanda ya Magharibi, imefanya ziara ya kuitambulisha kwa viongozi mbalimbali katika mikoa inayohudumia wakiwemo Wakuu wa Mikoa, Wilaya, Makamanda wa Polisi wa Mikoa hiyo, na taasisi inazoshirikiana nazo.

Baadhi ya wilaya zilizofikiwa katika mpango huo ni pamoja na Kigoma, Katavi na Tabora.

Ofisi ya EWURA Kanda ya Magharibi ilianza kazi tarehe moja Julai, 2023, na ofisi zake zipo katika mtaa wa Msigallo, Cheyo, Tabora.

Hadi sasa EWURA ina ofisi za Kanda sita, ambapo ofisi ya Kanda ya Ziwa inahudumia mikoa ya Mwanza, Simiyu, Geita, Mara na Kagera, Kanda ya Mashariki inahudumia Dar es Salaam, Pwani, Mtwara na Lindi na Kanda ya Kati inahudumia Dodoma, Morogoro, Singida na Iringa.

Nyingine ni Kanda ya Nyanda za Juu Kusini inayohudumia Mbeya, Songwe, Ruvuma na Njombe Kanda ya Kaskazini inayohudumua Arusha, Manyara, Tanga na Kilimanjaro ili kurahisisha utoaji wa huduma.

# Ushirikishwaji wa EWURA kwa wadau wa habari waleta mafanikio

***Na Tobietha Makafu***

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), hadi kufikia katikati ya mwaka huu wa fedha 2023/24, imewajengea uwezo wa kufahamu masuala ya kiudhibiti jumla ya waandishi wa Habari na wahariri nchini wapatao ... ili kufikisha taarifa sahihi kwa wananchi kupitia vyombo mbalimbali vya habari wanavyofanyia kazi.

Meneja wa Mawasiliano na Uhusiano EWURA, Bw. Titus Kaguo amesema hivi karibuni EWURA imekutana na Wahariri wa Vyombo vya Habari jijini Dar es Salaam na Lindi, Waandishi wa mikoa ya Kanda ya Kaskazini mkoani Arusha na waandishi wa mkoa wa Tabora.

Bw. Kaguo alisema EWURA hutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria ya EWURA, Sura Na. 414 ambapo Kifungu cha 6 (e)(i-iii) kinaitaka mamlaka hiyo kuboresha ustawi wa jamii kwa kuongeza maarifa na uelewa wa sekta, haki na wajibu wa watumiaji na watoa huduma zinazodhibitiwa, namna ya kusuluhisha malalamiko na migogoro, wajibu, kazi na shughuli za Mamlaka.

Katika mkutano na Wahariri wa vyombo vya habari jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Dkt. James Andilile alitoa mada kuhusu kazi, wajibu na changamoto zinazoikabili taasisi pamoja na mipango mikakati ya mbeleni.

"EWURA imedhibiti sekta ya nishati na maji kwa miaka 17 sasa, utendaji wake umekua na tija kwa jamii, ambapo tumetoa leseni kwa watoa huduma wa umeme, mafuta na mafundi umeme, tumefuta leseni kwa wasiotii masharti ya leseni, tumedhibiti uchakachuaji wa mafuta, tumefungua fursa za vituo vya mafuta vijijini na kutunza kanzi data ya watoa huduma wazawa katika miradi ya gesi na mafuta nchini na kuhakikisha ubora wa huduma zinazodhibitiwa kwa gharama halisi," alisema Dkt. Andilile.

Naye Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Nchini, Bw. Deodatus Balile, aliwapongeza EWURA kwa kuendeleza ushirikishwaji wa wadau wa habari kwani itawasaidia kuijua vyema sekta ya nishati na maji na kufikisha taarifa sahihi kwa wadau mbalimbali kupitia media.

EWURA imesema itaendelea kuboresha ushirikiano na wadau mbalimbali, wakiwemo wahariri na waandishi wa habari ili kuongeza uwazi katika kufanya kazi zake na kuwahabarisha wananchi moja kwa moja kupitia vyombo vya Habari.

# Mamlaka za Maji zatakiwa kuelimisha wateja kuhusu huduma

***Na Asiatu Msuya***

Mamlaka za Maji Nchini (WSSAs) zimetakiwa kuelimisha wateja wake kuhusu bei za huduma ya maji, mchakato wa kurekebisha bei, usomaji wa dira, matumizi sahihi ya maji na namna malalamiko ya wateja hao yanavyoshughulikiwa.

Mkurugenzi wa Maji na Usafi wa Mazingira EWURA, Mha. Exaudi Maro amesema EWURA imekua ikipokea malalamiko kutoka kwa wananchi na viongozi wa kisiasa kuhusu utekelezaji wa tozo mpya kwa baadhi ya Mamlaka za maji, jambo linalotia shaka kwamba huenda Mamlaka hazitoi elimu kwa kina kwa wateja wao kabla ya kutoza gharama mpya.

"Mchakato wa marekebisho ya bei na tozo huwa ni shirikishi na hufanyika kwa uwazi, na ni lazima kwa Mamlaka za maji kuwataarifu na kuwaelimisha wateja wao kabla na baada ya mchakato na daima wawe tayari kupokea na kutatua malalamiko ya wateja kwa wakati, hili pia limeainishwa katika kila agizo la tozo, hivyo tunatoa mwito kwa WSSAs kuzingatia," alisema Mha. Maro.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 28 cha Sheria ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2019 na Sheria ya EWURA Sura ya 414 2006, vinaipa mamlaka EWURA kudhibiti kiufundi na kiuchumi huduma za majisafi na usafi wa mazingira nchini, ili kulinda maslahi ya wadau; kuhakikisha uendelevu wa uwezo wa kifedha wa watoa huduma na kukuza upatikanaji wa huduma kwa watumiaji wote ikiwa ni pamoja na wa kipato cha chini.

Katika kufikia malengo hayo, EWURA, pamoja na mambo mengine, hutoa leseni, husimamia ubora na uhakika wa huduma, huidhinisha viwango na tozo. Zaidi ya hayo, EWURA hupitia upya mipango ya biashara, mikataba ya huduma kwa wateja, kukuza ushindani na ufanisi wa kiuchumi wa mamlaka hizo.

Kwa sasa, EWURA inasimamia jumla ya Mamlaka 81, kati ya hizo, 26 zinatoa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika makao makuu ya Mikoa, 43 makao makuu ya Wilaya, 5 Miji midogo na na 7 Miradi ya Kitaifa.



*Meneja wa EWURA Kanda ya Kaskazini, Mha. Lorivii Long'idu (aliyekaa katikati) katika picha ya pamoja na baadhi ya wadau wa habari wa mkoa wa Arusha, baada ya semina kwa wadau hao juu ya udhibiti wa huduma za nishati na maji.*